



## LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE

Justice Lugakingira House, Kijitonyama, P. O. Box 75254, Dar Es Salaam, TANZANIA  
Telephone: 2773048, 2773038, Fax: 2773037, E-mail: [lhrc@humanrights.or.tz](mailto:lhrc@humanrights.or.tz)  
Website [www.humanrights.or.tz](http://www.humanrights.or.tz)

### TAARIFA KWA UMMA KUHUSU KAULI YA WAZIRI MKUU JUU YA MCHAKATO WA KATIBA MPYA

Alhamisi Novemba 9, 2017

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kimesikitishwa na taarifa ya Serikali ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania iliyowasilishwa na Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa Novemba 9, 2017 kupitia mkutano wa tisa wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dodoma kusisitiza nia ya kutokuendeleza mchakato wa kupata katiba mpya kwa sasa.

*“Katiba mpya inahitaji gharama kubwa na sisi tumeanza na kutatua changamoto za jamii kwanza, ikiwemo mahitaji ya maji, changamoto za elimu, na sekta ya Afya”*. Alisema Waziri Mkuu Kassim Majaliwa.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinaitahadharisha Serikali kuwa jitihada za kupambana na ufisadi na kurejesha uwajibikaji hazitafanikiwa na kuwa endelevu bila uwepo wa katiba bora itakayoweka misingi ya utawala bora na usimamizi imara wa rasilimali za nchi. Masuala yaliyopewa kipaumbele na Serikali ya awamu ya tano yatakuwa na tija zaidi yatakapowekewa ulinzi wa kikatiba hasa kupitia Katiba inayotokana na maoni ya wananchi, hivyo basi mwendelezo wa mchakato wa Katiba ni muhimu zaidi kufanyika sambamba na utatuzi wa vipaumbele vya Serikali ya awamu ya tano.

Tukumbuke kuwa, mchakato wa Katiba Mpya katika hatua za awali umekwishagharimu kiasi cha pesa za kitanzania takribani **shilingi billion 100**, hivyo kwa kuuzika mchakato huu nchi itakuwa imepoteza kiasi hicho kikubwa cha pesa bila matokeo yoyote chanya.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, kinatoa wito kwa serikali kutokutumia visingizio vya gharama katika masuala ambayo yanagusa moja kwa moja maslahi ya kidemokrasia kwa wananchi. Serikali itambue kwamba hitaji la katiba mpya ni la wananchi na si la watawala.

Imetolewa na:

**Anna Henga (Wakili)**  
**Kaimu Mkurugenzi Mtendaji**

---

#### Board of Directors:

Prof. Geoffrey R.V. Mmari - Chairperson, Ms. Athanasia Soka(Adv) - Vice Chairperson, Dr. Helen Kijo-Bisimba - Secretary, Dr. Ringo W. Tenga (Adv) - Member, Mr. Francis Stolla (Adv) - Member, Ms. Emeline Mboya - Member, Ms. Pili Mtambalike - Member Mr. Thaddeo W. Mashera - Member